TANGAZO LA SERIKALI NA.147 la tarehe 3/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA YA 355)

---

# AMRI

---

*(Imetolewa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA SEKONDARI YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Sekondari ya Mwaka 2023.

Kutangaza Eneo la Upangaji
Sura ya 355

2. Eneo lililoloainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo lakwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa Mji wa Makambako.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo: -

"Mpaka unaanzia kwenye njiapanda, kati ya barabara za Mlowa na Manyerere kwenye majira - nukta 703081MS, 9021225KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki kwa kufuata barabara ya Mlowa kwa umbali wa kilomita 2.603 hadi kwenye majira – nukta 705199MS, 9019766KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa kufuata barabara inayoelekea Shule ya Sekondari ya Maguvani na mkondo wa maji ya mvua wa Igangidungu kwa umbali wa kilomita 1.664 hadi kwenye majira - nukta 704231MS, 9018521KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa kufuata mkondo wa maji ya mvua wa Igangidungu kwa umbali wa kilomita 2.397 hadi mahali ambapo mkondo wa maji ya mvua unakutana na barabara ya Manyerere kwenye majira - nukta 702589MS, 9020342KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini hadi barabara ya Manyerere kwa umbali wa kilomita 1.021 hadi ulipoanzia".

Dodoma
6 February, 2023

A. NGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi*